

SHULE YA SEKONDARI ADAM KIGHOMA MALIMA,

S.L.P 93,

RORYA.

TAREHE-----

JINA LA MWANAFUNZI-----

SHULE YA MSINGI-----

S.L.P-----

RORYA.

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ADAM KIGHOMA MALIMA:

01.UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Adam Kighoma Malima.**HONGERA SANA**.Shule hii ipo katika kijiji cha **Nyambori** katika kata ya **Bukura** tarafa ya **Nyancha** umbali wa **kilomita18** kutoka makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya **Rorya**.

Unatakiwa **kuripoti** shuleni kuanzia tarehe-----na **mwisho** wa kuripoti ni tarehe-----,ndani ya siku kumi na nne(14) usiporipoti nafasi yako yaweza kuchukuliwa na mwanafunzi mwingine.Na kushindwa kufika au kuripoti bila taarifa yoyote ya msingi kwa tarehe tajwa hapo juu ,hatua za kisheria na nidhamu zitachukuliwa dhidi yako(mwanafunzi),mzazi au mlezi.

02.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

(A) Mashati mawili aina ya tetroni/cotton meupe yenye mikono mifupi yawe na kola na mfuko upande wa kushoto

(B) Sweta rangi ya bluu kwa ajili ya baridi

(c) Suruali mbili **zenye tanapu,moja nyeusi na nyingine zambarau**.Epuka kununua au kushona suruali za **piston na modo haziruhusiwi kabisa(kwa wavulana)**

(D) Mkanda mweusi usiwe na chuma kikubwa au mapambo mengine

(E) Viatu vya ngozi **vyeusi** vya **kufunga na kamba** jozi mbili visiwe vya boot na kisigino kirefu na soksi jozi (1) **nyeusi** na jozi moja **nyeupe** wa wanafunzi wote.

(F) Sketi mbili aina ya tetron/cotton moja **nyeusi** na nyingine **zambarau, weka mistari mieupe miwili(ya zigzag) kwa mbele** kwenye sketi ya **zambarau** tu, marinda yawe ya kati yasiwe makubwa au madogo sana. **Sketi zote ziwe ndefu zinazofika kwenye kifundo cha mguu.**

(G)kiatu cha raba na **tracksuit(traksuti) nyeusi** ambazo zitavaliwa siku ya michezo

NB.Sare zote zitakaguliwa siku ambayo mwanafunzi ataripoti shuleni.

3.0 MAHITAJI MENGINE

a.Madaftari makubwa 10(counter book Q.2 kwa ajili ya nukuu za masomo

b.Mathematical set

c.Dictionary moja ya kiingereza kwa matumizi yake binafsi

d.Aje na ndoo ya lita 10 au fyekeo(kifaa kimoja wapo)

e.Afike na file folder(faili) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake

4.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NA PAMOJA NA;

1.Wizi

2.Uasherati,ubakaji na ushoga

3.Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya

4.Uvutaji bangi

5.Makosa ya jinai

6.Kupiga au kupigana

7.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

8.Kuoja au kuolewa

9.Kupata au kusababisha mimba ndani au nje ya shule

10.Kutoa mimba

11.Kudharau bendera ya taifa

12.kugoma,kuchochea au kuongoza fujo,migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule

13.Kukataa adhabu kwa makusudi

14.Kukutwa na simu ndani au nje ya shule

5.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu ,sayansi,teknolojia na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ya msingi na muhimu;

a. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

b.Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

c.kuwahi katika kila shughuli za shule ikiwa ni pamoja na **mchakamchaka asubuhi**

d.Kufahamu mipaka ya shule na kuiheshimu kwani kuwepo nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya uongozi wa shule ni kosa kubwa.Hivyo heshimu mipaka ya shule kipindi chote cha uanafunzi wako.

MUHIMU:1. RATIBA YA SHULE YETU HUANZA KILA SIKU ZA KAZI SAA MOJA(1:00) ASUBUHI

2.FOMU ILIYOANDIKWA "MEDICAL EXAMINATION FORM" SHARTI IJAZWE NA DAKTARI ANAETAMBULIWA NA SERIKALI.

KARIBU SANA

WAKO

MRONI ELIAS

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
ADAM KIGHOMA MALIMA S.S.
P.O.Box 93 SHIRATI-RORYA

0621 450 119, 0789 679 874, 0758 07 18 18

ADAM KIGHOMA MALIMA SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

MKUU WA SHULE
ADAM KIGHOMA MALIMA S.S.
P.O. Box 93 SHIRATI-RORELE

Full name-----

Age-----Height(in cm)-----Weight-----

1.Blood count----- (red and white)-----

2.Stool Examination-----

3.Urinalysis-----

4.T.B and Leprosy test-----

5.Symlias and other V.D-----

6.Eye test-----

7.Ears-----

8.Chest-----

9.Abdomen-----

10.Plano-test(girls)-----

11.Spleen-----

Additional information;example physical defects or impairment, infections,chronic or family diseases(e.g sicle cell) and inability to eat certain food etc

I certify that the above named student is fit/is not fit to persue Secondary Education

Signature-----Date-----

Disignation-----Station-----